## Somo la kwanza: Uoni na matatizo mbalimbali ya uoni

- Uoni wa karibu ni uwezo wa kuona vitu vilivyo karibu
- Uoni wa mbali ni uwezo wa kuona vitu vilivyo mbali
- Matatizo ya Uoni yanayoweza kuepepukika, kupunguzwa makali au kurekebishwa kabisa kwa kutumia matibabu na/au vifaa saidizi
- Matatizo ya Uoni yanayoweza kuepukika yanasababishwa na matitizo ya Afya ya Macho na tatizo la kuona mbali/karibu
- Tatizo la kuona mbali/karibu ni tatizo lililoko kwenye umbo la jicho. Hii inaweza kusababisha:
    - **Myopia:** Mtu ana shida ya kuona vizuri vitu vya mbali
    - **Hyperopia:**
        - Vijana wenye hyperopia ya kiwango cha kati wanapata ugumu kuona vitu vilivyo karibu.
        - Vijana wenye hyperopia kali wanapata ugumu kuona vizuri vitu vilivyo karibu na vilivyo mbali
        - Watu wazima wenye hyperopia wanapata ugumu kuona vitu vilivyo mbali na vilivyo karibu.
    - **Astigmatism:** Mtu anapata ugumu kuona vizuri vitu vilivyo karibu na vilivyo mbali
    - **Presbyopia:** Mtu mwenye umri zaidi ya miaka 40 anapata ugumu kuona vizuri vilivyo karibu
- Matatizo ya macho yasiyoweza kuepukika hayawezi kurekebishwa kwa kutumia matibabu. Matatizo haya yanajumuisha Uoni wa kiwango hafifu na Upofu. Baadhi ya vifaa saidizi vinaweza kusaidia watu walio na matatizo ya macho yasiyoweza kuepukika, kufanya vitu wanavyotaka kufanya.

## Somo la pili: Vifaa Saidizi vya Uoni

- Vifaa Saidizi vya Uoni ni pamoja na:
    - Vifaa ambavyo vinaweza kumsaidia mtu mwenye Uoni hafifu au kuboresha Uoni (kwa mfano: miwani ya kusomea, miwani iliyoshauriwa na daktari, vioo kuza, vifaa vya kuona mbali)
    - Vifaa ambavyo vinaweza kusaidia mtu mwenye Uoni hafifu au upofu kutumia uwezo wao wa kuhisi au kugusa kufanya kazi (Kwa mfano: breli na stylus, audio players, Saa zinazotoa sauti pale zinapoguswa)
    - Vifaa vinaweza kumsaidia mtu mwenye Uoni hafifu au Upofu kusogea (Kwa mfano: Fimbo nyeupe)
- Mtu anaweza kutumia kifaa Saidizi kimoja au zaidi ya kifaa kimoja, kwa kulingana na mahitaji yake na kazi anazotaka kufanya.
- Baadhi ya vifaa saidizi vinajumuishwa kwenye TAP na baadhi havijumuishwi ( mfano miwani ambayo imeshauriwa na daktari) kwa vile inahitaji mtu mwenye stadi za kiwango cha juu na vifaa vyenye uwezo mkubwa ili kuweza kutoa miwani ya aina hiyo.

## Somo la tatu: Namna ya kufanya kipimo rahisi cha Uoni

- Kipimo cha Uoni cha TAP sio tathmini kamili ya Uoni. Ni kipimo cha kujua kama mtu ana tatizo la macho au ugumu katika kuona na kama:
    - Anapaswa kupewa rufaa kwenda kumuona mtaalam wa Tiba ya Macho au daktari.
    - Anapaswa kuelekezwa kutumia miwani iliyoshauriwa na daktari.
    - Anaweza kufaidika na vifaa saidizi vya Uoni vilivyojumuishwa kwenye TAP

- Fomu ya Kipimo cha Uoni cha TAP inaelekeza upimaji na inajumuisha:
  - Upimaji rahisi wa Afya ya Macho- kusaidia kuainisha dalili za jicho lisilokuwa na afya sahihi.
  - Vipimo rahisi vya Uoni wa mbali na karibu- ili kusaidia kuanisha matatizo ya kuona yanayoweza kutokea.

| **Mambo ya kufanya kwa kulingana na matokeo ya Kipimo rahisi cha Uoni:** | |
|---|---|
| **Toa rufaa** kwenda kwa Mtaalam wa tiba ya Macho ili Uchunguzi zaidi ufanywe kwa mtu ambaye**:** | • Ana dalili za kuwa na jicho lenye afya hafifu, maumivu ya jicho au hali ya kutokujisikia vizuri.<br>• Ana ugonjwa wa kisukari<br>• Hawezi kusoma herufi ndogo za E wakati wa kipimo cha Uoni wa Umbali mrefu ( lakini anaweza kuona E za kati na E kubwa) na bado hajaenda kumuona Mtaalam wa TIba ya Macho kwa siku za hivi karibuni.<br>• Hawezi kuona herufi za E wakati wa kipimo cha Uoni wa Karibu na ana umri zaidi ya miaka 35. |
| **Chagua** miwani ya kusomea kwa mtu ambaye: | • Hawezi kuona herufi E kwenye kipimo cha Uoni wa karibu, lakini ana Uoni wa Umbali mrefu na ana umri zaidi ya miaka 40 |
| **Chagua(au toa rufaa)** aina ya vifaa saidizi kwa uoni hafifu kwa mtu ambaye: | • Hawezi kuona herufi E kwenye kipimo cha umbali mrefu na amemuona Mtaalam wa Tiba ya Macho kwa siku za hivi karibuni.<br>• .Hawezi kuona herufi E wakati wa kipimo cha Uoni wa karibu; miwani ya kusomea haimsaidii; na amemuona Mtaalam wa Tiba ya Macho kwa hivi karibuni. |